**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

***Dar es Salaam***
***14 Agosti, 2025***

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema Tuzo aliyokabidhiwa na Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani (CISM) ni heshima kwa Watanzania wote na ni msukumo wa kuimarisha michezo ndani ya Majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo leo Ikulu wakati wa hafla ya kutunukiwa Tuzo hiyo iliyowasilishwa kwake na Makamu wa Rais wa CISM na Mkuu wa Mafunzo ya Ulinzi na Operesheni wa Jeshi la Ulinzi la Nigeria, Meja Jenerali Maikano Abdullahi.

CISM imetoa tuzo hiyo ikiwa ni ishara ya kutambua mchango wake katika kuliwezesha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kushirikiana kimataifa katika maendeleo ya michezo ya majeshi na kusimamia misingi ya amani, mshikamano, urafiki, usawa, uadilifu na ushupavu.

Rais Dkt. Samia amesema kuwa majukwaa ya michezo ya kijeshi ni nyenzo muhimu ya kujenga mshikamano wa kijeshi unaovuka mipaka ya kijiografia na tofauti za kimila na kitamaduni, sambamba na kuchochea urafiki na kuaminiana miongoni mwa vikosi vya ulinzi na usalama Barani Afrika.

Ameongeza kuwa fursa kama hizi zinapaswa kuendelezwa kwa maslahi mapana ya majeshi na maendeleo ya michezo kwa ujumla.

Akizungumzia umuhimu wa mazoezi kwa afya katika kuepusha magonjwa yasiyo ya kuambukizwa, Rais Dkt. Samia amezitaka Wizara, Taasisi na Mashirika ya Serikali kushiriki kikamilifu katika mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), akisisitiza umuhimu wake katika kujenga Taifa lenye afya.

Katika hatua nyingine, Rais Dkt. Samia amempongeza Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob John Mkunda kwa kufanikisha Mkutano Mkuu wa 79 wa CISM uliofanyika nchini Tanzania na kushuhudia ushiriki wa wageni mbalimbali.

Aidha, Rais Dkt. Samia amesema Serikali italifanyia kazi ombi la CISM la kuandaa mashindano ya kimataifa ya michezo ya majeshi nchini Tanzania.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu